# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

# TAARIFA KWA UMMA

## UTARATIBU WA KUTOA VIBALI VYA KUSAFIRISHA SAMAKI NA MAZAO YA UVUVI NDANI NA NJE YA NCHI

Tanzania imebahatika kuwa na maeneo mengi ya maji ambamo kuna rasilimali nyingi za uvuvi yakiwemo maji baridi na Bahari ya Hindi, maziwa ya kati na madogo, mabwawa ya asili, mito na maeneo oevu. Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepewa jukumu la kusimamia ipasavyo rasilimali za uvuvi hapa nchini.

Aidha, Wizara inayo Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015 inayolenga kuwepo kwa usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Utekelezaji wa Sera ya Uvuvi unazingatia Sheria ya Uvuvi Sura ya 279, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009, na marekebisho yake ya mwaka 2018, 2019, 2020 na Kanuni za Maabara za mwaka 2012 kama zilivyofanyiwa marekebisho ya mwaka 2015.

Vilevile, Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015 imefafanua majukumu ya taasisi mbalimbali zikiwemo Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma, Taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) na wadau.

Miongoni mwa majukumu ambayo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza ni kutoa vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi (Permit for movement of fish and fishery products). Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Kanuni ya 93(6) na (7) zinaelekeza utaratibu wa utoaji wa vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi.

Hata hivyo, hivi karibuni imebainika kuwa vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi vimekuwa vikitolewa na watu wasiohusika (Unauthorised officers) na jukumu hilo kinyume cha Sheria, wakiwemo Maafisa Uvuvi wasioruhusiwa katika ngazi za Halmashauri, wenyeviti wa vitongonji, vijiji, watendaji wa kata na maafisa tarafa kinyume cha Sheria na Kanuni za uvuvi. Hali hii imesababisha uvunjaji wa sheria na hivyo kuwasababishia wavuvi na wafanyabiashara wa samaki na mazao ya uvuvi kupata hasara na kuleta mkanganyiko katika jamii. Vilevile, utoaji wa vibali usiozingatia taratibu zilizowekwa umesababisha upotevu wa mapato ya Serikali katika ngazi za Halmashauri na Serikali Kuu na kuongeza mianya ya utoroshaji wa mazao hayo kinyume cha Sheria.

Katika kudhibiti jambo hilo, Wizara inautangazia umma wa watanzania kuhusu utaratibu sahihi wa utoaji wa vibali hivyo. Kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Sura ya 279 Kifungu 5 (1), Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009, Kanuni ya 93(6) zinaelekeza utaratibu wa kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi kutoka eneo la uvuvi (mialo) kwenda kwenye masoko ya ndani ya nchi. Aidha, Kanuni za Uvuvi, Kanuni ya 95 (2) hadi (4) inatoa utaratibu wa kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi.

Kutokana na ukiukwaji wa utoaji wa vibali ulioelezwa hapo juu, Wizara inautangazia Umma wa Watanzania kwamba utaratibu sahihi wa kutoa vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi ni kama ifuatavyo: -

1. Kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Sura 279 Kifungu cha 5(1) vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi ndani ya wilaya na mkoa vitatolewa na Afisa uvuvi aliyeruhusiwa (Authorised Officer) aliyepo katika Halmashauri husika;
2. Vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi nje ya mkoa au nje ya nchi vitatolewa na Maafisa Uvuvi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Sura 279 Kifungu 5(1) na Kanuni za Uvuvi, Kanuni ya 93(6) na (7) na 95 (2) hadi (4). Orodha ya Maafisa Uvuvi wa Wizara walioruhusiwa waliopo katika maeneo mbalimbali nchini imeambatishwa pamoja na Tangazo hili;
3. Aidha, Maafisa Uvuvi waliokuwa wameruhusiwa kutoa vibali vya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi kabla ya tangazo hili wamesitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Sura 279 Kifungu 4 (3), Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009, Kanuni ya 146 (4).
4.

Hivyo, wafanyabiashara na wadau wote wa uvuvi wanashauriwa kuzingatia utaratibu huu, unaolenga kutatua changamoto zilizokuwepo kuhusiana na utoaji wa vibali vya usafirishaji wa samaki na mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi. Maafisa Uvuvi walioteuliwa kutekeleza kazi hii watakuwa na vitambulisho maalumu. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Maafisa Wafuatao: -

1). Ezra K. Mutagwaba - Simu Na. 0655 390 476,
2). Stephen A. Lukanga – Simu Na. 0754 437 234;
3). Merisia S. Mparazo - Simu Na. 0787 217 651

### MAJINA YA MAAFISA UVUVI WALIOTEULIWA KUWA WATOA VIBALI VYA KUSAFIRISHA SAMAKI NA MAZAO YA UVUVI KITAIFA NA KIMATAIFA

| Na | Jina la Kituo | Majina ya Watumishi Walioteuliwa | Cheo | Namba ya Simu | Eneo la kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Ziwa Victoria (2) | 1. Roman J. Mkenda | Afisa Uvuvi I | 0714 036 070 | Kanda ya Ziwa Victoria |
| | | 2. Prosper A. Mremi | Afisa Uvuvi Mwandamizi | 0763 064 405 | Kanda ya Ziwa Victoria |
| 2 | Bukoba (4) | 1. Samson Mabala Mboje | Afisa Uvuvi I | 0765 298 428 | Mkoa wa Kagera |
| | | 2. Johnbosco C. Rubajuna | Mtekinolojia wa Samaki Mwandamizi Msaidizi | 0756 827 495 | Wilaya za Bukoba, Ngara na Misenyi |
| | | 3. Theresia R. Temu | Mtekinolojia wa Samaki Msaidizi Mkuu | 0784 121 518 | Wilaya za Bukoba, Ngara, Misenyi |
| | | 4. Stanslaus F. Rwezaura | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0783 564 586 | Wilaya za Bukoba, Ngara, Misenyi |
| 3 | Musoma (4) | 1. Yohana C. Mirumbe | Mtekinolojia wa Samaki | 0786 710 734 | Mkoa wa Mara |
| | | 2. Julieth Albert Kituku | Mtekinolojia wa Samaki Mwandamizi | 0713 847 682 | Mkoa wa Mara |
| | | 3. Deogratius Mobasi Mgabo | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0766 233 110 | Wilaya za Musoma, Tarime, Butiama, Serengeti na Rorya |
| | | 4. Mkinze R. Mkinze | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0754 539 347 | Wilaya za Musoma, Bunda |
| 4 | Rorya | 5. Gosberth M. Buchard | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0625 814 659 | Wilaya za Tarime, Butiama, Serengeti na Rorya |
| 5 | Muleba (2) | 1. Masanja Lucas Kadashi | Afisa Uvuvi Mkuu Msaidizi | 0742 796 604 | Wilaya ya Muleba |
| | | 2. Nankondo Elisante Senzira | Afisa Uvuvi Mkuu | 0754 882 511 | Wilaya ya Muleba |
| | | | | | |
| 6 | Geita (2) | 1. Gabriel M. Mageni | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0768 193 139 | Mkoa wa Geita |
| | | 2. Benedicto Magonda Mathias | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0754 237 772 | Wilaya ya Geita, Chato, Nyang'wale |
| 7 | Sengerema (2) | 1. Oswald John Alonga | Afisa Uvuvi | 0763 480 888 | Wilaya ya Sengerema/ Buchosa |
| | | 2. Daudi Juma Kadashi | Afisa Uvuvi Mkuu Msaidizi | 0754 988 549 | Wilaya ya Sengerema/ Buchosa |
| 8 | Mwanza (4) | 1. Hamad John Stima | Afisa Uvuvi Mkuu | 0769 753 022 | Mkoa wa Mwanza |
| | | 2. Dorina Dalali Mlenge | Afisa Uvuvi | 0755 576 569 | Wilaya ya Nyamagana, Ilemela |
| | | 3. Humphrey Herry Tillya | Afisa Uvuvi Mwandamizi | 0655 317 575 | Wilaya ya Nyamagana, Ilemela |
| | | 4. Lusuka Nichrous Lusuka | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0754 042 260 | Wilaya ya Nyamagana, Ilemela |
| 9 | Ukerewe (3) | 1. Derrick Deo Kajuna | Afisa Uvuvi Mkuu Msaidizi | 0746 861 033 | Wilaya ya Ukerewe |
| | | 2. Zacharia E. Maya | Mtekinolojia wa Samaki Mkuu Msaidizi | 0620 248 096 | Wilaya ya Ukerewe |
| | | 3. Keya Manyansi Masore | Mtekinolojia wa Samaki Mkuu Msaidizi | | Wlaya ya Ukerewe |
| 10 | Simiyu (3) | 1. Jacomina Jacob Ntundu | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0752 067 999 | Mkoa wa Simiyu |
| | | 2. Mohamed Said Ngauna | Mhandisi Mitambo Baharini Mwandamizi | 0783 126 834 | Wilaya za Magu, Bariadi, Busega, Meatu, Itilima, Maswa |
| | | 3. Peter Edmond Mndolwa | Nahodha II | 0653 526 229 | Wilaya ya Magu, Bariadi, Busega, Meatu, Itilima, Maswa |
| 11 | Kigoma (3) | 1. Agnely Adrian Lishela | Afisa Uvuvi Mkuu | 0655 537 179 | Kanda ya Ziwa Tanganyika |
| | | 2. Kisaka Suedi Kimaro | Nahodha I | 0752 828 405 | Wilaya za Kigoma na Kasulu, Kalambo |
| | | 3. Frank Festo Kabitina | Mtekinolojia wa Samaki Mkuu | 0756 258 991 | Wilaya za Kigoma, Kasulu |
| | | 4. Abdul Mohamed Ghandai | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0759 904 455 | Wilaya ya Kalambo |
| 12 | Buhingu (2) | 1. Laurent Sylivester Kabuche | Mtekinolojia wa Samaki Msaidizi | 0628 551 340 | Wilaya ya Uvinza, Tanganyika |
| | | 2. John I. Mzee | Mhandisi Mkuu (PMT) | 0629 133 600 | Wilaya ya Uvinza |
| 13 | Kipili (2) | 1. Kasberth Mohamed Raphael | Nahodha | 0757 335 829 | Wilaya ya Nkasi. |
| | | 2. Rashid Jonas Juma | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0754 489 367 | Wilaya ya Nkasi. |
| 14 | Kasanga (2) | 1. Gaspar R. Lugelelo | Afisa Uvuvi | 0769 774 154 | Wilaya za Kalambo na Sumbawanga |
| | | 2. Geofrey Manfred Salaka | Nahodha | 0756 606 451 | Wilaya za Kalambo, Nkasi Sumbawanga |
| 15 | Ikola (2) | 1. Dominick Chobaliko Milenguko | Mtekinolojia wa Samaki Msaidizi | 0754 403 339 | Wilaya za Tanganyika, Mpanda, na Mlele |
| | | 2. Dickson Oswald Juvenary | Mhandisi (MT) | 0753 530 362 | Mkoa Katavi - Tanganyika, Mpanda na Wilaya |
| 16 | Tunduma (2) | 1. Francis Lazaro Mpatama | Afisa Uvuvi Mkuu | 0755 339 274 | Mkoa wa Songwe, Wilaya za Momba, Mbozi, Mji mdogo wa Tunduma. |
| | | 2. Bahari Elias David | Afisa Uvuvi Mkuu Msaidizi | 0766 192 704 | Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Momba na Mbozi |
| 17 | Kasumulu (2) | 1. Marko N. Nzungu | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0755 894 445 | Wilaya za Kyela, Tukuyu na Ludewa. |
| | | 2. Rowland Gibson Mcharo | Mtekinolojia wa Samaki Mwandamizi Msaidizi | 0752 267 740 | Wilaya za Kyela, Tukuyu na Ludewa. |
| 18 | Rukwa (1) | 1. Msabaha A. Kashindi | Nahodha II | 0759 382 868 | Wilaya za Songwe na Momba, na Mlele. |
| 19 | Mtera Dam (1) | 1. Hamis Mohamed Petta | Mtekinolojia wa Samaki Msaidizi | 0626 870 413 | Wilaya za Mpwapwa, Chamwino na Iringa. |
| 20 | Mbamba Bay (2) | 1. Erica Robert Mathayo | Afisa uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0692 439 659 | Wilaya za Nyasa, Songea na Namtumbo. |
| | | 2. Jerome J. Fundi | Afisa uvuvi Mwandamizi | 0715 725 173 | Wilaya za Nyasa, Songea na Namtumbo. |
| 21 | D, Salaam (4) | 1. Mathayo Bakari Werema | Afisa Uvuvi | 0676 996 844 | Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na Kilimanjaro. |
| | | 2. Jovice J. Mkuchu | Mtekinolojia wa Samaki Mkuu | 0755 758 989 | Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Tanga na Kilimanjaro. |
| | | 3. Mfaume Jabir Balozi | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0753 933 334 | Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Bagamoyo na Mkuranga,. |
| | | 4. Emmanuel Deus Kwilasa | Afisa Uvuvi | 0753 999 164 | Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Bagamoyo na Mkuranga, |
| 22 | Namanga (2) | 1. Christina Aaron Maganga | Afisa Uvuvi Msaidizi Mwandamizi | 0755 984 638 | Mkoa wa Arusha, Mkoa Manyara |
| | | 2. Joseph Stanslaus Kulagwa | Afisa Uvuvi Msaidizi I | 0762 048 420 | Mkoa wa Arusha, Mkoa Manyara |
| 23 | Tanga (2) | 1. Jacob M. Nalaila | Afisa Uvuvi Mkuu Msaidizi II | 0653 854 620 | Wilaya za Tanga, Muheza, Pangani, Mkinga) |
| | | 2. Frida G. Mndambi | Mtekinolojia wa Samaki Mkuu Msaidizi | 0692 626 339 | Wilaya za Tanga, Muheza, Pangani na Mkinga |
| | | 3. Violatha B. Masolwa | Afisa Uvuvi Mkuu | 0762 070 314 | Horohoro & Mkinga |
| 24 | N/Mungu (2) | 1. Godbless Ngetwa Msuya | Muunda Boti Mkuu (PBB) | 0654 270676 | Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. |
| | | 2. William James Muguhi | Nahodha Mkuu (PSKP II) | 0621 369 287 | Wilaya za Moshi, Simanjiro, Mwanga. |
| 25 | Mafia (2) | 1. Magesa Majigo Nyambele | Nahodha Mkuu (PSKP I) | 0715 057 913 | Wilaya ya Mafia |
| | | 2. Hamis Shedrack Mkaga | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0688 767 877 | Wilaya ya Mafia |
| 26 | Kilwa (3) | 1. Michael Amir Makundi | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0714 355 612 | Wilaya ya Kilwa |
| | | 2. Veronica C. Miti | Afisa Uvuvi | 0742 800 153 | Wilaya ya Kilwa |
| | | 3. Ramadhan Abdallah Mvugilije | Afisa Uvuvi Msaidizi | 0764 793 447 | Wilaya ya Kilwa |
| 27 | Mtwara (2) | 1. Emeritha B. Saulo | Afisa Uvuvi Mwandamizi Msaidizi | 0717 649 268 | Mikoa ya Mtwara & Lindi |
| | | 2. Shilinde Andrew Nzungu | Mtekinolojia wa Samaki | 0655 280 910 | Mkoa wa Mtwara |
| 28 | Singida (2) | 1. Joseph Lyaga Mbaga | Afisa Uvuvi | 0769 639 627 | Mikoa ya Singida, Tabora |
| | | 2. Godlove Thomas Donkoli | Mtekinolojia wa Samaki Msaidizi | 0786 205 178 | Mikoa ya Singida, Tabora |
| 29 | Dodoma HQ (3) | 1. Kimasa W. Bugomba | Afisa Uvuvi Mkuu II | 0713 383 011 | Mikoa ya Dodoma na Morogoro |
| | | 2. Hamady Timoth Makorwa | Afisa Uvuvi | 0719 757 818 | Mikoa ya Dodoma na Morogoro |
| | | 3. Emanuela X. Mawoko | Afisa Uvuvi Mkuu II | 0752 919 689 | Mikoa ya Dodoma na Morogoro |
| | | 4. Hamida Ngala Mbwana | Fisheries Officer I | 0685 703 009 | Mikoa ya Dodoma na Morogoro |
| | | 5. Julieth Evance Mwaipungu | Fisheries Officer I | 0718 291 854 | Mikoa ya Dodoma na Morogoro |
| | **JUMLA YA MAAFISA WOTE: 72** | | | | |

Imetolewa na: -

**Dkt. Rashid A. Tamatamah,**
**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi),**
**S.L.P 2847, 40487 DODOMA.**
**Baruapepe: barua@uvuvi.go.tz**

SQ006580